**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

# WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI

# (RITA)

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA TAKWIMU TANZANIA BARA



## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Serikali kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kusajili matukio muhimu ya binadamu ambayo ni vizazi, vifo na sababu zake, ndoa, talaka na watoto wa kuasili. Ili kuboresha hali ya usajili nchini Serikali ilifanya tathmini ya kina na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Habari na Uwajibikaji wa Afya ya Mama na Watoto *(Commission on Information and Accountability for Women's and Children's Health - COIA)* ambayo Mwenyekiti Mwenza alikuwa ni Mheshimiwa Dk. Jakaya Mrisho Kikwete Rais mstaafu wa awamu ya nne na Stephen Harper aliyekuwa Waziri Mkuu wa Kanada. Pendekezo la kwanza la tume hiyo lilikuwa "*Ifikapo mwaka 2015, nchi zote ziwe zimechukua hatua madhubuti ya kuanzisha Mfumo wa usajili wa vizazi, vifo na sababu zake utakaooanisha Mfumo huo na mfumo mzuri wa taarifa za afya kutoka katika vituo vya tiba, taarifa za kiutawala pamoja na tafiti*"

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Pendekezo hili lilichukuliwa na Kikao cha Pili cha Mawaziri wenye Dhamana ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu wa Afrika, ambao walitaka kila nchi ya Afrika kuchukua hatua za haraka katika kuboresha Mifumo ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu. Aidha, mkutano wa tatu ulisisitiza juu ya kuboresha Mifumo ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu kwa kutangaza mwaka 2015 hadi 2024 kama muongo mmoja wa kuboresha mifumo hiyo barani Afrika kuwa na lengo la kuhakikihsa "hakuna kuacha mtu nyuma" *("leave no one behind").*

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Pamoja na hayo, maandalizi ya Mkakati huu yamezingatia vipaumbelele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Mkakati umelenga kuangalia masuala ya Mfumo wa Usajili, kupitia Sheria ya Usajili, kuboresha Mfumo wa Tehama na kuimarisha mahusiano baina ya Taasisi zinazohusika na majukumu ya usajili.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Pia, Mkakati huu umelenga kuboresha hali ya usajili na upatikanaji wa uhakika wa takwimu za matukio muhimu ya binadamu. Hatua hii itawezesha Serikali kuimarisha mifumo yake ya maendeleo katika nyanja za uchumi, jamii, siasa, ulinzi na usalama. Vilevile, Mkakati huu unalenga kuboresha hali ya usajili wa matukio ya vifo (na sababu zake) ili nchi iweze kuchukua hatua stahiki kuzuia vifo hivyo.

## 1. HALI ILIVYOKUWA

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108 inaweka usajili kuwa ni suala la lazima kwa kila mtu. Pamoja na sheria kuweka ulazima huo bado Taifa liliendelea kuwa na mfumo usioridhisha wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu hususan kwa upande wa Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kupata takwimu sahihi/muhimu kwa ajili ya maendeleo kutokana na kukosekana kwa utaratibu thabiti wa usajili hususan vizazi na vifo. Hivyo, kutekelezwa kwa Mkakati huu kunasaidia Serikali kupunguza gharama za uendeshaji na kuwezesha upatikanaji wa haraka wa takwimu sahihi na muhimu kwa ajili ya mipango ya maendeleo na kuimarisha hali ya usalama katika nchi yetu.

## 2. ATHARI ZILIZOTOKEA

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Athari za kuwa na mfumo dhaifu wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu ni nyingi, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa matumizi makubwa ambayo yangeweza kuepukika katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kukosekana kwa takwimu za uhakika kwa ajili ya kuandaa mipango ya maendeleo ya Taifa katika sekta mbalimbali kama vile elimu, afya, huduma ya maji, mipango miji na usambazaji wa nishati. Athari nyingine ni ukosefu wa maendeleo ya familia na jamii kwa ujumla, mwenendo wa ongezeko la watu, mahitaji mahsusi ya jamii, hali ya ulinzi na usalama wa nchi.

## 3. MALENGO MAHSUSI YA MKAKATI

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Lengo kuu la Mkakati huu ni kuongeza kiwango cha usajili nchini kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kwa kuwa na Mfumo unaojitosheleza wa Usajili wa Matukio Muhimu ya

Binadamu na Takwimu kwa kusajili matukio yote ya vizazi katika miezi sita katika vituo vya tiba na Ofisi za Kata. Vilevile, kuhakikisha makundi mengine yanasajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa hivyo kuhakikisha kila mwananchi aliyezaliwa Tanzania Bara anatambulika kwa kuwa na cheti cha kuzaliwa hadi kufikia 2025.

## 4. MISINGI YA MKAKATI

**Mheshimiwa Mwenyekiti: Misingi ya Mkakati huu ni pamoja na:**

i. Kupeleka huduma ya usajili karibu na wananchi kupitia Sera ya Ugatuzi wa Madaraka kwenye serikali za mitaa ili kuongeza kiwango cha usajili kwa kusogeza huduma karibu na wananchi na kupunguza gharama.

ii. Kurejea mfumo wa kisheria na mifumo ya kitaasisi ili kuweza kuendana na mabadiliko ya kimfumo yanayotokana na utekelezaji wa Mkakati huu.

iii. Kutengeneza mfumo wa uratibu utakaohakikisha ushiriki wa wadau wote kwa suala hili mtambuka.

## 5. UTEKELEZAJI WA MKAKATI

### 6.1. MAFANIKIO

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Mkakati huu ulianza kutekelezwa mwaka 2013 kama ifuatavyo:

#### i. Kusogeza Huduma za Usajili Karibu na Wananchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Wakala umesogeza huduma za usajili karibu na wananchi kwa kushusha usajili kwenye vituo vya tiba na Ofisi za Kata, ambapo huduma za usajili wa vizazi zinatolewa katika mikoa 18 hadi sasa. Mikoa hiyo ni Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara, Simiyu, Dodoma, Singida, Ruvuma, Morogoro, Pwani, Tanga na Kilimanjaro. Hatua hii imesaidia masuala yafuatayo:

a) Kuongeza vituo vya usajili kwa kufanya vituo vya tiba na ofisi za kata kuwa ni vituo vya usajili. Hii inamaanisha watoto katika mikoa 18 ambapo mfumo huu

unatekelezwa wanaweza kusajiliwa karibu kabisa na sehemu wanazoishi;

b) Wananchi kupata muda mwingi zaidi wa kufanya shughuli nyingine za maendeleo kwa kuwa muda uliokuwa unatumika kufuatilia vyeti vya kuzaliwa mbali na maeneo yao ya makazi umepungua;

c) Watendaji wa TAMISEMI katika mikoa hiyo wamewezeshwa kwa kupewa mafunzo na vitendea kazi ili kuwezesha zoezi la usajili kufanyika kwa ufanisi;

d) Hatua za usajili zimeweza kurejewa na kufanya usajili kuwa wa papo kwa hapo na kuondoa hatua nyingi zilizokuwepo hapo awali;

e) Serikali imeondoa ada hivyo kuwezesha watoto wote walio na umri chini ya miaka mitano kusajiliwa na hivyo mtoto wa mwananchi wa kawaida kusajiliwa bila ya kipingamizi cha ada;

f) Jamii imeendelea kupewa elimu juu ya umuhimu wa usajili na kuwa na cheti cha kuzaliwa; na

g) Wakala umeweza kupata taarifa za usajili pindi tu mtoto anaposajiliwa ambapo taarifa hizo hutumwa kwenye kanzi data ya Wakala kwa kupitia simu janja.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Kwa ujumla kusogeza huduma karibu na wananchi kumesaida kupandisha kiwango cha usajili kutoka iliyokuwa asilimia 13% hadi kufika 55% kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano.

Mafanikio hayo makubwa ya utekelezaji wa mkakati huu yameainishwa katika jedwali namba1 kama ifuatavyo;-

Jedwali 1: Kiwango cha Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano wenye vyeti vya kuzaliwa Tanzania Bara, 2020

| Mkoa | Makadirio ya Idadi ya watoto (Agosti, 2018)* | Idadi ya Watoto Wenye Vyeti vya Kuzaliwa (Septemba, 2020)** | % ya Watoto Wenye Vyeti vya kuzaliwa |
|---|---|---|---|
| Dodoma[π] | 377,724 | 328,944 | 87.1 |
| Arusha | 295,585 | 95,841 | 32.4 |
| Kilimanjaro[π] | 213,142 | 221,041 | 103.7 |
| Tanga[π] | 348,378 | 341,151 | 97.9 |
| Morogoro[π] | 373,012 | 347,329 | 93.1 |
| Pwani[π] | 175,123 | 203,646 | 116.3 |
| Dar es Salaam | 740,034 | 468,532 | 63.3 |
| Lindi[π] | 118,877 | 103,779 | 87.3 |
| Mtwara[π] | 181,900 | 154,314 | 84.8 |
| Ruvuma[π] | 233,003 | 216,023 | 92.7 |
| Iringa[π] | 138,022 | 137,819 | 99.9 |
| Mbeya (na Songwe)[π] | 497,130 | 378,342 | 76.1 |
| Singida[π] | 274,125 | 231,184 | 84.3 |
| Tabora | 508,011 | 40,301 | 7.9 |
| Rukwa | 239,859 | 11,005 | 4.6 |
| Kigoma | 474,273 | 38,310 | 8.1 |
| Shinyanga[π] | 319,536 | 184,705 | 57.8 |
| Kagera | 543,833 | 24,291 | 4.5 |
| Mwanza[π] | 596,613 | 175,144 | 29.4 |
| Mara | 384,049 | 300,705 | 78.3 |
| Manyara | 303,432 | 21,584 | 7.1 |
| Njombe[π] | 97,939 | 100,914 | 103.0 |
| Katavi | 135,728 | 3,522 | 2.6 |
| Simiyu[π] | 352,050 | 240,097 | 68.2 |
| Geita[π] | 399,143 | 231,504 | 58.0 |
| **Tanzania Bara** | **8,286,429** | **4,600,029** | **55.5** |

[π]Mikoa inayotekeleza Mpango wa Usajili wa Watoto Wenye Umri wa Chini ya Miaka Mitano (U5BRI)

*Makadirio yameafanywa na RITA kulingana na kiwango cha kuongezeka wa watu (population growt rate) kwa kila mkoa

**Idadi inajumuisha watoto wote waliosajiliwa kwenye mifumo ya ki-elekroniki ya RITA pamoja na idadi ya fomu ambazo hazijaingizwa kwenye mifumo ya ki-elekroniki

## Marejeo ya Sheria

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo Sura ya 108 ili kuweka mazingira wezeshi ya kisheria katika ugatuaji wa shughuli za usajili na matumizi ya TEHAMA. Marekebisho yamefanyika kupitia Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 4 ya mwaka 2019 pia kanuni zinazotokana na marekebisho hayo zinaendelea kufanyiw kazi. Marejeo haya yameakisi mabadiliko yaliyokuwa yanaendelea kufanyika katika kushusha huduma za usajili karibu na wananchi katika ngazi ya kata na vituo vya tiba na hivyo kuongeza kiwango cha usajili. Haya ni mafanikio makubwa kwani hapo awali maboresho hayo yalikuwa yanafanyika kwa kupitia Hati ya Makubaliano baina ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Ninapenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa kusimamia na kuwezesha marekebisho haya ya Sheria.

### ii. Usajili wa Vizazi vilivyochelewa kuandikishwa

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Ili kuweza kuhakikisha kiwango cha usajili kinaongezeka na pia kuondoa bakaa ya watu wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa ikiwa ni sehemu ya Mkakati huu, Wakala umesogeza huduma ya usajili kwa watoto wenye umri wa miaka 5 hadi 17 walio katika mfumo wa elimu na wale walio nje ya mfumo wa elimu, pamoja na vizazi vyote vilivyochelewa kuandikishwa kwa kuhakikisha wanasajiliwa kupitia Shule wanazosoma au Ofisi za Kata. Usajili huu hushirikisha waratibu wa elimu kata na ofisi za Makatibu Tawala wa Wilaya. Hadi sasa jumla ya wanafunzi 478,177 wamesajiliwa katika wilaya 29 kama zinavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Namba 2: Idadi ya wanafunzi waliosajiliwa katika wilaya kwa kupitia mfumo huu wa usajili.

| Na | Wilaya | Idadi ya Halmashauri | Idadi ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 1 | NJOMBE | 3 | 37,732 |
| 2 | LUDEWA | 1 | 16,446 |
| 3 | MAKETE | 1 | 10,848 |
| 4 | WANGING'OMBE | 1 | 18,854 |
| 5 | ILALA | 1 | 11,323 |
| 6 | KINONDONI & UBUNGO | 2 | 6,477 |
| 7 | KIGAMBONI | 1 | 3,513 |
| 8 | TEMEKE | 1 | 21,364 |
| 9 | IRINGA | 1 | 563 |
| 10 | KILINDI | 1 | 2,013 |
| 11 | MUSOMA | 2 | 49,295 |
| 12 | BARIADI | 3 | 18,215 |
| 13 | TARIME | 2 | 32,414 |
| 14 | SINGIDA | 2 | 19,139 |
| 15 | SONGEA | 3 | 11,954 |
| 16 | BUNDA | 2 | 24,769 |
| 17 | MASWA | 2 | 20,849 |
| 18 | KAHAMA | 3 | 21,741 |
| 19 | MANYONI | 2 | 13,234 |
| 20 | MNAZI MMOJA-ILALA | 5 | 24,328 |
| 21 | CHALINZE-BAGAMOYO | 1 | 5,236 |
| 22 | SENGEREMA | 2 | 6,759 |
| 23 | BABATI | 2 | 10,828 |
| 24 | GEITA | 2 | 67,864 |
| 25 | MISUNGWI | 1 | 3,120 |
| 26 | ARUSHA | 1 | 13,090 |
| 27 | ILEMELA | 1 | 2,969 |
| 28 | NYAMAGANA | 1 | 2,362 |
| 29 | MLELE | 1 | 878 |
| **Jumla** | | **29** | **478,177** |

### iii. Maboresho ya Mfumo wa Usajili kutumia TEHAMA

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Wakala umeboresha Usajili kwa kutumia TEHAMA kupitia mfumo mpya wa Usajili wa Vizazi na Vifo kwenye Teknolojia mpya ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na hivyo kuongeza uwezo na kuhakikisha kunakuwa na ubadilishanaji taarifa na Taasisi nyingine. Hadi sasa mfumo wa Wakala kupitia mradi wa "Birth Registration Fourth Generation" (BRS4G), umeunganishwa na mifumo ya taasisi za serikali zikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa-NIDA na UHAMIAJI kwa lengo la kubadilishana na kuhakiki taarifa za vizazi na vifo kwa matumizi ya ofisi. Aidha, wadau wengine wanatarajiwa kuunganishwa katika mfumo huu ni; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya-NHIF, Bodi ya Mikopo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi-NEC, na Baraza la Mitihani Tanzania-NECTA.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma zake za usajili kwa kutumia mtandao (E-Huduma) ulianza rasmi kutumika mwezi Juni, 2020. Mfumo wa usajili kwa kutumia mtandao (E-Huduma) umeendelea kuboreshwa na kuwezesha wananchi kupata huduma mbalimbali zikiwemo; maombi mapya ya vizazi na vifo, uhakiki wa vyeti vya vizazi na vifo na kubadili vyeti vya kuzaliwa na vifo. Hadi kufika mwezi Februari, 2021 jumla ya maombi 119,129 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Jumla ya vyeti vya kuzaliwa na kifo 117,377 vya wanafunzi wanaoomba mikopo katika Bodi ya Elimu ya juu vilihakikiwa kupitia mfumo huu kwa lengo la kutambua uhalali wake. Aidha, maombi 1,741 yalihusu vyeti vya kuzaliwa na vifo na maombi 11 yalihusu ubadilishaji wa vyeti vya zamani kwenda vyeti vipya.

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Kutokana na maboresho haya, sasa vyeti vya kuzaliwa na vifo vinatolewa papo kwa papo katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Lugalo, , Mbagala Round Table, Mnazi Mmoja, Kairuki, Kinondoni, Chanika, Mbagala Rangi Tatu, Vijibweni, Sinza Palestina, Mbande, Bukombe, Bulegela, Uyovu, Buzirayombo, Bwanga, Chato, Nzera, Katoro, Kasamwa, Geita, Masumbwe, Iboya, Nyijundu, Kharumwa, Mwendakulima, Kahama, Bulungwa, Chela, Lunguya, Nhobola, Kishapu, Ng'homango, Salawe, Ihalo, Songwa, Kolandoto, Shinyanga.

## 6.2. CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA USAJILI

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Changamoto za utekelezaji wa Mkakati huu wa Usajili ni pamoja na;

i. Uhaba wa watumishi katika ngazi mbalimbali. Kwa kuwa ili kuweza kutekeleza mkakati huu kwa ufanisi kunahitaji rasilimali watu, Wakala unahitaji kuwa na Waratibu wa Mikoa na Wilaya.

ii. Jamii kutokuwa na majina ya watoto pindi wanapozaliwa ili kuwezesha mzazi kupata cheti pindi anapozaliwa.

## 6.3 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Katika kutatua changamoto hizo Wakala umekuwa ukitoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa usajili na kupata cheti cha kuzaliwa na kifo na pia kujiandaa na majina ya watoto. Pia Wakala umeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Tamisemi kwa kuwatumia watendaji katika vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto pamoja na ofisi za kata, japo bado katika ofisi za Wilaya bado tunauhitaji.

# 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Mwenyekiti:** Suala la usajili wa matukio muhimu ya binadamu ni la kisheria na linaweka msingi wa kukuza na kulinda haki za binadamu. Hivyo, kuendelea kutekelezwa kwa Mkakati huu kutasadia kuimarika kwa hali ya usimamizi na utekelezaji wa sheria za nchi na uzingatiwaji wa haki za binadamu na kupungua kwa gharama za uendeshaji katika kutafuta na kupata taarifa za watu kutokana na mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa. Vilevile, Mkakati huu unaiwezesha Serikali kuwa na mipango mahsusi na jumla inayoongozwa na uhalisia wa takwimu za watu na matukio katika jamii na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa sensa ya watu na makazi, zoezi linalogharimu kiasi kikubwa cha fedha.

**Dashibodi ya usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano inasaidia kupata takwimu za usajili wa watoto kulingana na jinsi (ME/KE), mahali kizazi kilipo sajiliwa (Kituo cha Tiba/ Ofisi ya Mtendaji Kata), mahali kizazi kilipotokea (Kituo cha Tiba/ nyumbani), kiwango cha usajili kwa vipindi tofauti (siku, mwezi, mwaka) pamoja na kiwango cha usajili katika ngazi ya mbalimbali (Mkoa, Halmashauri, Kata na Kituo ch Tiba).**

